KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 14, Issue 1

4th Shawwâl 1432

2nd Sept, 2011

YALIYOMO

UTEREMSHO "WAHYI" 1 - 3

UMUHIMU WA SUNNAH 3 - 4

UTEREMSHO "WAHYI", MBALI NA QUR'ÂN

Na: The Qur'an and Sunnah Society of East Africa [QSSEA]

Qur'aan ni neno la Allaah aliloteremshiwa Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) na kuhifadhiwa na Maswahaba zake kwa njia ya ki-matamshi na ki-maandiko. Mbali na Qur'aan, jambo jengine lolote alilotamka au alilotenda Mtume (صلى الله عليه وسلم) vilevile limehifadhiwa na Maswahaba. Hivyo basi, Sunnah inajumuisha misemo (au maneno) ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), inayojulikana kwa jina mashuhuri la Hadeeth, mwenendo wake, na vitendo alivyo-viidhinisha yeye mwenyewe.

Qur'aan na Sunnah ni zenye kujulikana chini ya kichwa cha anwani "Wahy" وحي - uteremsho"); tafauti baina ya vitu viwili hivi ni kwamba Qur'aan ni uteremsho unao somwa, na haliyakuwa Sunnah si uteremsho wenye kusomwa. Umuhimu wa Sunnah kama chimbuko la pili ya Uislamu umeelezwa kwenye Faslu ya pili.

Mwanzo kabisa, tutathibitisha hapa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم), hakuwa akiteremshiwa aya za Qur'aan peke yake kutoka kwa Allaah (Subhaanau wata'aalah), bali alikuwa akiteremshiwa uteremsho (wahyi) mara kwa mara ambao sasa umehifadhiwa katika Hadeeth. Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi Qur'aan yenyewe inavyojihusisha na uteremsho huu.

Kulingana na aya ya 144 ya Soorah al-Baqarah, Allaah (Subhaanau wata'aalah), amemuamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم), aielekee Ka'bah katika Swala zake za kila siku badala ya kuelekea Jerusalem.

"Kwa yakini tukiona unavyogeuzageuza uso wako mbinguni. Basi tutakugeuza kwenye Kibla ukipendacho. Basi geuza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu (Al-Ka'bah); na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko (msikiti huo)…"

Lakini, ni kwa nini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akielekea Jerusalem kabla ya hapo? Aya ya 143 yaonyesha yakwamba Allaah Mwenyewe ndiye aliyeichagua Jerusalem kuwa ndicho Kibla cha Mtume (صلى الله عليه وسلم): **"…na hatukukifanya Kibla ulichokuwa nacho (mara ya kwanza kuwa ndiyo kibla chako sasa na mpaka mwisho wa ulimwengu) ila upate kumjulisha (atambulikane) yule anayemfuata Mtume na yule anayegeuka akarejea nyuma…"** Kuchaguliwa kwa kibla kilichotangulia kumetajwa kumaanisha kuwa hilo ni jambo lililopita. Lakini hakuna aya katika Qur'aan inayomuamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) aelekee Jerusalem mwanzoni mwa ulinganizi wake! Kwahivyo, ni lazima ifahamike hapa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliupata uongofu huu (wa kuelekea Jerusalem) kutoka kwa Allaah kwa njia isiyokuwa Qur'aan. Kama tulivyoeleza hapo awali yakwamba, uteremsho huu wa njia nyengine umehifadhiwa katika Sunnah. Katika aya ya 3, Soorah at-Tahreem, kuna mkasa fulani ulisimuliwa: **"Na wakumbushe wakati Mtume alipomwambia mmoja wa wake zake jambo la siri;** (na yule mkewe akalitangaza). Basi (mke yule) alipolitangaza, na Allaah akamdhihirishia (Mtume wake kuwa huyu bibi ameitangaza siri). Mtume alimjuvya (huyu bibi) sehemu ya yale (aliyoyasema) na akaacha sehemu nyengine. Basi alipompasha (mkewe) habari hii, alisema (yule mkewe): "Nani aliyekupa habari hii?" (Mtume) akasema: "Amenipa habari hii yule aliye mjuzi (wa kweli), Mwenye habari (ya kila jambo)." Ni lazima tukizingatie kifungu hiki cha maneno: na Allaah akamdhihirishia (Mtume wake kuwa huyu bibi ameitangaza siri); na: Amenipa habari hii yule aliye mjuzi (wa kweli), Mwenye habari (ya kila jambo). Suali hapa ni kwamba, Allaah alimjuvya na kumwambia kwa njia gani? Hapana shaka yakwamba, njia hiyo haikuwa ya Qur'aan, kwani tukio hilo halikutajwa popote katika Qur'aan. Kwahivyo, ni lazima Mtume (صلى الله عليه وسلم) awe ameelezwa maneno hayo kwa njia nyengine (ya uteremsho) isiyokuwa ya Qur'aan.

NENO LA BUSARA

"Siku moja, Ummul Mu'mineen (Mama yao Waumini) 'Aaisha (رضي الله عنها) aliulizwa: "Ilikuwaje tabia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)?" Nae akajibu, "Tabia yake haikuwa chochote isipokuwa ni Qur'aan".

Katika aya 5 ya Soorah al-Hashr, kumetajwa kisa cha safari ya jeshi lililoandaliwa kwenda kupambana na kabila la Mayahudi la Banu Nadir lililo asi, ambapo waislamu waliikata baadhi ya mitende na kuyaacha mengine: **"Mtende wowote mlioukata (katika hicho kiambo cha Mayahudi) au mliouacha umesimama vilevile katika mashina yake; yote haya ni kwa idhini ya Allaah; (hapana lawama juu yenu); na kwa kuwadhalilisha wavunjao Sharia."**

Hapa, vitendo vyao vimetokana na "idhini ya Allaah" waliyopewa. Hapana mahali popote katika Qur'aan

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

ilipotolewa ruhusa hiyo. Kwahiyo, Allaah alimuongoza Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika kisa hiki, lakini haikuwa kwa kupitia Qur'aan.

Kulingana na aya za 17-18 za Soorah al -Qiyaamah, Allaah aliahidi kuikusanya Qur'aan Yeye Mwenyewe. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaamrisha waandishi wa Qur'aan wazipange soorah (hizo za Qur'aan) kama zinavyopatikana hii leo; Haikuteremshwa (Qur'aan) katika mpangilio huu. Kwahivyo, kwa vile jukumu hili lilikuwa ni la Allaah, basi yaonyesha yakwamba Yeye ndiye aliyemuongoza Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) kuhusiana na mpangilio huo wa soorah za Qur'aan.

Hii ni baadhi ya mifano michache miongoni mwa mifano mengi yenye kuondoa tashwishi yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiteremshiwa wahyi kutoka kwa Allaah, emma kwa njia ya moja kwa moja au kwa kupitia kwa Jibreel. Sehemu ya wahyi huo ulihifadhiwa neno kwa neno chini ya anwani ya "Qur'aan". Aina nyengine zote za wahyi zilijumuishwa, emma kwenye matamshi yake (صلى الله عليه وسلم) au kwenye nyenendo zake zilizohifadhiwa vyema na maswahaba zake kama Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم).

MATAKWA MBALI-MBALI YENYE KUHUDUMIKIWA NA SUNNAH:

Siku moja, Ummul Mu'mineen (Mama yao Waumini) 'Aaisha ((رضي الله عنه aliulizwa, "Ilikuwaje tabia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)?" Nae akajibu, "Tabia yake haikuwa chochote isipokuwa ni Qur'aan". Kwahivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa ni mfano halisi wa Qur'aan yenyewe. Kila alichokuwa akifanya au akisema, yaani: Sunnah, ina uhusiano mkubwa na Qur'aan. Hebu sasa tufanyeni utafiti katika uwajibu wa Sunnah kuhusiana na Qur'aan.

SUNNAH HUFAFANUA ZAIDI MAAMRISHO YA QUR'AAN.

Allaah amesema katika aya ya 43 ya Soorah al-Baqarah: **"Simamisheni Swala na mutoe zaka",** na aya nyengine nyingi kama hizo zinapatikana.

Mas-ala yote yanayohusiana na swala, kama vile idadi inayohitajika ya swala za kila siku, idadi ya *raka'aat* na visomo katika kila swala, na vilevile jinsi ya kuitekeleza swala yenyewe kuanzia mwanzo hadi mwisho wake, (yote hayo) yamefafanuliwa na Sunnah. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم); "Swalini kama mulivyoniona mimi nikiswali." (*imepokelewa na Bukhari*)

Vile-vile, mas-ala yote yanayohusiana na Zakaah, k.m (*kwa mfano*); uchache wa kiwango anachohitajika kuwa nacho mwenye kulipa, asili-mia inayolipwa, aina ya utajiri, bidhaa, na wanyama wenye kuwapasa kutolewa Zakaah n.k (*na kadhaalika*); (hayo) yameelezwa *parwanja*(waziwazi) katika Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Na pia, ukamilifu wa miondoko ya Hajj na kufunga Saumu yanaweza kuonekana katika Sunnah, kwani Qur'aan imeyataja mas-ala mawili haya kwa mukhtasar tu.

Amesema Allaah katika Soorah al-Maaidah, aya ya 38; **"Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao; malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu, itokayo kwa Allaah. Na Allaah ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima."** [Soorah al-Maaidah 5:38]

Sunnah hufafanua kiwango cha chini cha/uchache wa bidhaa za kuibwa zenye kumpasa mwivi adhabu na jinsi itakavyostahiki mkono huo kukatwa. Kuikanusha Sunnah hiyo, kama wafanyavyo baadhi ya "Waislamu" wapotofu (*wanaodhani kuwa wao ni watetezi wa haki za ki-Binadamu*), kutaifanya Qur'aan nzima kuwa ni mkusanyiko wa tafsiri zenye kutokamana na *Hawaa* na mawazo ya wengine ambayo chanzo chake ni mashetani. Kwa mfano, mtu asiyekubali kuidhihirisha swala yake ki-utendaji kama ilivyofundishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), atakuwa akiicheza-shere swala hiyo kwa kuiswali kulingana na mapendelewa yake. Lakini, kwani Muislamu atamuabudu vipi Allaah, ikiwa hajui jinsi ambayo Allaah Mwenyewe anavyotaka kuabudiwa?

SUNNAH INAWEZA KUTHIBITISHA MAANA MAKHSUSI IWAPO KUNA UWEZEKANO WA MAANA ZAIDI YA MOJA.

Allaah amesema katika aya ya 82 ya Soorah al-An'am: "(Hapana shaka kuwa) wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na dhulm (ushirikina) kuwa hao ndio watakaopata amani, nao ndio walioongoka."

Imaam al-Bikhaari akahadithia hapa yakwamba baadhi ya maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walilifasiri neno dhulm kwa maana yake ya ki-ujumla, yaani kudhulumu, kufanya makosa. Kwahivyo likawakera jambo hilo kisha wakajiuliza, "Ni nani miongoni mwetu ambae hajawahi kufanya makosa?" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaondolea kero hilo kwa kuwafahamisha yakwamba maana ya neno "dhulm" katika ayah hii ni kufanya shirk, kama ilivyo kwenye Soorah Luqmaan aya ya 13; **"Kwa hakika kumshirikisha Allaah ndiyo dhuluma kubwa."**

Allaah akasema katika Soorah at-Taubah, aya ya 34-35: **"Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Allaah, wape habari za adhabu inayoumiza (inayowangoja). Siku (mali yao) yatakapotiwa moto katika moto wa Jahannam, na kwa hayo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao…"**

Maana ya hili neno la kiarabu ((كنز "kanz" ni (mirundiko ya) akiba, mikubwa au midogo. Kwahivyo ayah hii inamuhukumu mtu yoyote mwenye kurundika mali yenye thamani ya kiwango chochote bila ya kutumia kwa njia ya Allaah. Kwa kuitafakari maana hii katika akili zetu, 'Umar (رضي الله عنه) alimuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu ayah hii nae akamjibu yakwamba pindi kile kiwango cha deni la Zaka likishalipwa, huwa haitambuliki tena kuwa ni "kanz". (Ibn Maajah)

HADEETH HUFAFANUA MATUKIO YA KI-HISTORIA KIUKAMILIFU KWA VILE MATUKIO HAYO HUELEZWA KWA MUKHTASAR KATIKA QUR'AAN.

Amesema Allaah katika soorah al-Anfal aya ya 7: **"Na (kumbukeni) Allaah alipokuahidini moja katika mataifa mawili ya kwamba ni lenu. Nanyi mkapenda mupate lile lisilo na nguvu; na Allaah anapenda kuthubutisha haki kwa maneno yake na (anapenda) kuikata mizizi ya makafiri."**

Ni mataifa yapi hayo mawili yaliyokusudiwa? Na ni taifa lipi lilokuwa halina silaha? Ni kutoka kwenye vitabu vya ahaadeeth tuliposimuliwa kwa ukamilifu kuhusiana na vita vya Badr; navyo ndivyo vita vilivyokusudiwa kwenye aya hiyo iliyotangulia.

Soorah at-Tawbah, aya ya 118 yasema; **"Na (pia akawaelekea kwa rehema) wale watatu waliongojeshwa (kukubaliwa toba yao kwa yale makosa yao makubwa waliyoyafanya)."**

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Ni kina nani hawa watu watatu, na ni kwa nini walibakia nyuma? Vilevile vitabu vya ahaadeeth vimeyasimulia hayo.

Soorah 'Abasa, aya ya 1-2: **"Alikunja uso na akapa nyongo. Kwa sababu alimjia kipofu."**
Ni nani huyo aliyekunja uso na akapa mgongo?, na ni kwa nini? Ni nani huyo aliyekuwa kipofu? Bila ya shaka ukamilifu wa matukio hayo yamesimuliwa na vitabu vya ahaadeeth.

SUNNA INAWEZA KURUHUSU MAMBO FULANI KUTOKA KATIKA AMRI YA MAKATAZO KWA UJUMLA.

Kwenye Soorah an-Nisaa' aya ya 11, fungu la watoto katika mirathi limetajwa. **"Allaah anakuusieni juu ya watoto wenu …"**
Mtume (صلى الله عليه وسلم) akatufafanulia yakwamba watoto wafuatao hawawezi kurithi:

1. mtoto muislamu wa mzazi asiekuwa muislamu (kafiri).
2. mtoto asiekuwa muislamu (kafiri) wa mzazi muislamu.
3. Na mtoto mwanamke au mwanamume mwenye kumuuwa babake.

Qur'aan imepasisha yakwamba nyamamfu na damu zimeharamishwa (*Haraam*) katika soorah al-Maidah aya ya 3. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaruhusu samaki na nzige kutoka katika neno "nyamamfu", na pia maini na mawengo kutoka katika neno "damu".

MAKISIO YA MIFANO YENYE MAKATAZO KATIKA MAMBO YANAYOSHABIHIANA.

Soorah an-Nisaa' aya ya 23: "Na (mmeharamishiwa kuwaoa) madada wawili wakati mmoja…"
Mtume (صلى الله عليه وسلم) vilevile amethibitisha yakwamba ni haraam kumuowa mwanamke pamoja na shangazi yake katika wakati mmoja. Tembo limethibitishwa kuwa ni haraam na Allaah (*Subhaanahu wata'aalah*) katika Soorah al-Maidah aya ya 93. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaurefusha uharamu huo na kuingiza ndani yake kila chenye kulevya kwa wingi, hata kama mtu atatumia kwa uchache.

MTUME (صلى الله عليه وسلم) AMEZIDISHA MAKATAZO KWENYE IDADI YA MAS'ALA TAFAUTI.

Miongoni mwa mambo mengi yaliyokuwa yakimshughulisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) ilikuwa ni kuwafahamisha waumini ni lipi lililo halaal na lipi lililo haraam (Soorah al-A'raaf, aya ya 157). Kwa mfano, aliharamisha kula nyama ya punda, mbwa, wanyama wenye meno yaliyochongeka na ndege mbua (wenye kuwinda k.m. tai). Vilevile ameharamisha dhahabu na hariri kwa waislamu wanaume, lakini akawahalalishia

UMUHIMU WA SUNNAH

Hapana Muislamu yoyote wa kweli awezae kuthubutu kwenda kinyume na mafundisho ya Qur'aan na Sunnah, lakini ni jambo la kusikitisha sana kuona yakwamba baadhi ya wapenda "maendeleo na mabadiliko" miongoni mwa waheshimiwa katika jamii hujitokeza na vifua mbele juu ya mwito yakwamba kitabu cha Allaah chatutosha sisi na wala hatuna haja na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) . Utakuta yakwamba miito kama hii hutangazwa na watu wenye malengo ya kufutilia mbali Sheria za ki-Islamu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa kitambo akijua yakwamba watu wa aina hiyo wenye malezi yenye mafunzo mabaya watakuja miongoni mwetu. Hivyo basi, akatutahadharisha kuhusiana na uovu huo kama ilivyopokewa na Al-Miqdam bin Ma'di Karib, mmoja wa Maswahaba: **"Kwa hakika mimi nimepewa Qur'aan na kitu chengine mfano wake. Baadae kutakuja wakati ambapo mtu aliyejitegemeza kwenye kochi lake atakaposema, 'Fuateni Qur'aan peke yake: muonacho kuwa ni halaal hapo (katika Qur'aan), basi kifanyeni kuwa ni halaal, na muonacho kuwa ni haraam hapo (katika Qur'aan), kifanyeni kuwa ni haraam.' Lakini kwa hakika, aliyoyakataza Mtume** (صلى الله عليه وسلم) **ni kama aliyoyakataza Allaah."** (Abu Daawud, Daarimi).

Kwa hakika, MTU YOYOTE MWENYE KUKATAA SUNNAH ZA MTUME (صلى الله عليه وسلم), (MTU HUYO) HAIAMINI QUR'AAN, kwani Allaah Mwenyewe ameusisitiza umuhimu wa Sunnah katika aya nyingi sana, zikiwemo miongoni mwazo, hizi zifuatazo.

59. Enyi mlio amini! Mt'iini Allaah, na mt'iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume, ikiwa mnamuamini Allaah na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema.

65. La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenykee kabisa.

Ikapokewa kutoka kwa Anas yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "***Nimewawachia miongoni mwenu vitu viwili; kamwe hamutopotea iwapo mutashikamana navyo; Kitabu cha Allaah na Sunnah zangu."*** (Haakim).

Walikuwa maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakishikamana kwa ta'dhima kubwa sana na amri zitokazo kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), wakawa hawazitafautishi na amri zitokazo kwa Allaah (*Subhaanahu wata'aalah*). Siku moja 'Abdullaah ibn Mas'ood (*radhiallaahi 'anhu*) aliismulia hadeeth hii alipokuwa akitoa khutbah, ***"Allaah na awalaani wanawake wenye michoro ya chale (tattoo) miilini mwao na wale wenye kuchonga nyusi zao; na wale wenye kutengeneza mwanya kwenye meno yao ili waonekane kuwa ni warembo na wale wenye kubadilisha maumbile ya Allaah."*** Maneno hayo yakamfikia mwanamke mmoja wa kabila la Banu Asad aitwae Umm Ya'qoob. Akamfuata 'Abdullaah ibn Mas'ood (radhiallaahi 'anhu) na akamwambia, "Ewe Abu 'Abdur-Rahmaan! Zimenifikia khabari mimi yakwamba wewe umewalaani wanawake fulani na fulani." Akasema: "Na ni kwanini mimi nisiwalaani wale ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) amewalaani na pia waliolaaniwa katika Kitabu cha Allaah." Akasema (Umm Ya'qoob): "Mimi nimeshasoma kila kilichomo baina ya magamba mawli." Akamjibu 'Abdullaah ibn Mas'ood (رضي الله عنه): "Lau kama ungelikuwa ni msomaji mzuri, basi ungeliyagundua hayo. Kwani wewe hukusoma aya ifuatayo?
Kuna mifano mingi sana kutoka kwa maswahaba ionyeshayo jinsi wanavyojikokoteza katika kuandama Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) mpaka kufikia hadi ya kukatana vizazi pindi wakigundua yakwamba pana mtu anaejaribu kwenda kinyume na Sunnah. Hebu tuangalie baadhi ya mifano katika maisha ya Makhalifa wakubwa wa Ki-Islamu na kisha kufuatiwa na kundi la maswahaba wengine.

Baada ya kifo cha Mtume (صلى الله عليه وسلم), Ummah wa ki-Islamu ulikabiliwa na mambo matatu makubwa. Nusra mambo hayo yangeliwatenganisha Waislamu lau

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

kama si uongofu mwema wa Sayyidna Abu Bakr (رضي الله عنه) ambae aliyewatuliza kwa amani chini ya muangaza wa Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Tatizo la kwanza lilihusiana na kuchaguliwa kwa Khalifa. Walipojumuika kwenye Saqifa Bani Sa'ida, kundi kubwa la Muhajireen na Ansaar walijishughulisha na ugomvi kuhusu tatizo hili. Ansaar wakapendekeza yakwamba AMIR na achaguliwe kutoka katika jumuiya zote mbili. Sayyidna Abu Bakr (رضي الله عنه) akahadithia maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba: "ma-Imamu watakuwa ni kutoka kwenye Kabila la Quraish maadamu watakuwa na ufahamu (wa dini)." Ansaar wakaikubali hoja hiyo na wakawa watulivu. Sayyidna 'Umar (رضي الله عنه) akalipendekeza jina la Abu Bakr (رضي الله عنه) kuwa awe ni Khalifa, na likaungwa mkono shaurio hilo bila ya kupingwa na wale waliokuwepo mahali pale na kisha baadae wakafuata wakaazi wa Madina kwa kumbay'I (kula kiapo cha utiifu).

Tatizo la pili likawa ni kuhusu mahali atakapozikwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwa mara nyengine tena, Abu Bakr (رضي الله عنه) akahadithia maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba: "Mtume huzikwa mahali avutapo pumzi zake za mwisho." Uamuzi ukakatikiwa kulingana na shauri hilo na mazishi yakafanywa katika chumba chake alichokufia cha mkewe, Ummul Mu'mineen. 'Aaisha (رضي الله عنها).

Tatizo la tatu ni suala la urathi wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama lilivyo daiwa na mwanae Faatimah (رضي الله عنها). aliyekuja kwa Sayyidna Abu Bakr (رضي الله عنه) kudai fungu lake. Abu Bakr (رضي الله عنه) akamjibu kwa kumkumbusha maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba: "Sisi, jamii ya Mitume, haturithiwi. Kitu chochote tuachacho nyuma yetu ni sadaqa". Faatimah (رضي الله عنها) hakuleta ugomvi zaidi na badala yake akarudi nyuma kimya.

Siku moja Sayyidna 'Umar (رضي الله عنه) alimuona Khalid ibn al-Waleed (رضي الله عنه) amevaa shati la hariri. Akamuomba alivue shati hilo. Khalid akamjibu yakwamba hata 'Abur-Rahmaan ibn 'Awf (رضي الله عنه) pia nae analo shati kama hilo. 'Umar (رضي الله عنه) akasema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimruhusu yeye kwa sababu alikuwa akiugua maradhi mabaya ya muasho." Kisha Khalid (رضي الله عنه) hakuwa na la kufanya isipokuwa kulivua shati hilo.

Baada ya kupata habari za ushindi wa Waislamu kwenye ukombozi wa Syria, 'Umar (رضي الله عنه) akasonga mbele kuelekea Damascus pamoja na idadi kubwa ya maswahaba. Alipofika pambizoni mwa 'Amwas, kijiji kilichoko Syria, habari za kuenea kwa ugonjwa wa *Tauni* mjini zikamfikia. 'Umar (رضي الله عنه) akawataka shauri watu wake iwapo wabahatishe kuingia humo mjini. Mjadala uliopamba moto ulitulizwa wakati 'Abdur-Rahmaan Ibn 'Awf alipohadithia maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba: "Ukiweko mahali ambapo magonjwa ya mlipuko (*epidemic*) yamezagaa, usitoke nje ya hapo. Na wala usende hapo iwapo ulikuwa mbali na mahali hapo." Hatimae, 'Umar (رضي الله عنه) akawaamuru wenzake waachane na kwenda mahali hapo. Mtu mmoja akamaka na akasema: "Ewe 'Umar, kwani wewe wakimbia kutoka kwenye maja'aliwa yaliyokadiriwa na Allaah?" Nae 'Umar (رضي الله عنه) akamjibu: "Naam, twakimbia kutoka kwenye Qadar moja hadi nyengine katika maja'aliwa ya Allaah vilevile."

Hivyo ndivyo ilivyokuwa hikma ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kwa *Qarne* nyingi zilizopita ikatuonyesha dalili zilizopo za kileo za kanuni za hifadhi dhidi ya maradhi (*Quarantine*). Siku moja Sayyidna 'Uthmaan (رضي الله عنه) alikubali kununua sehemu ya ardhi kutoka kwa mtu fulani. Baada ya kumaliza maafikiano yao kwa matamshi matupu, akamwambia yule mtu achukuwe pesa zake siku iliyofuata. Lakini yule mtu akaja baada ya masiku kadhaa akiwa amebadili msimamo waliokuwa wameafikiana. Alibadilisha kauli yake baada ya marafiki zake kumlaumu kwa kuuza ardhi yake kwa bei duni. 'Uthmaan (رضي الله عنه) angelikataa kata-kata kuhusu kubadili maafikiano yao, haswa kwa vile walikuwa tayari wamesha-afikiana kikamilifu. Lakini aliyakumbuka maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yenye kumpenda mtu mwenye kuwahudumia watu kwa ulaini na kwa moyo mkunjufu katika biashara zake. Kwahivyo, 'Uthmaan ((رضي الله عنه alimridhia yule jamaa matakwa yake bila ya kuzua ugomvi wowote.

Siku moja Sayyidna 'Alee (رضي الله عنه) alifuatwa na mtu mmoja aliyemtaka ampe naseeha kuhusu posa ya binti yake aliyetakwa na watu watatu: Hassan, Hussein, na 'Abdullah bin Ja'far: Sayyidna 'Alee (رضي الله عنه) akajikuta kuwa yeye binafsi ni muhusika mkubwa hapo kwa vile watoto wake wawili ni miongoni mwa wagombezi. Lakini akayakumbuka matamshi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yasemayo, "Mwenye kuombwa naseeha, na awe muadilifu." Basi baada ya kutuliza fikra zake, akamwambia yule mtu: 'Usende kwa Hassan kwa sababu yeye anajulikana sana kwa kuwaacha wake zake mara kwa mara. Na wala usende kwa Hussein kwa vile yeye anapenda kujipendekeza sana. Na badala yake nenda kwa 'Abdullah bin Ja'far.'

Katika mojawapo ya misafara yake, Sayyidna 'Alee (رضي الله عنه) alimkuta mfanyi biashara mmoja aliyehodhi (*aliyerundika*) mirundiko ya nafaka kwa kutarajia faida kubwa. Sayyidna 'Alee (رضي الله عنه) akamkumbusha maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mwenye kurundika mali (kwa njia hii) amelaaniwa", kisha akaamuru itolewe adhabu na watu wake kwa kuzichoma bidhaa hizo. Hivi ndivyo walivyokuwa ma-Khulafaa wanne walivyoshikamana na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Hebu tuangaze katika mifano mengine katika maisha ya maswahaba. 'Abullaah ibn Mas'ud alimsikiya mtu akisema baada ya kuchemua: "Al-hamdu Lillaah was Salaatu was Salaamu 'Ala Rasoolullaah." Ibn Mas'ud akamwambia: 'Yote uloyasema ni ya kweli. Lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakutufundisha hivyo. Alituamrisha tuseme 'Al-hamdu Lillaah' tu, baada ya kuchemua. Ni jambo bora kuwakumbusha ndugu zetu kuhusu Sunnah hii iliyo-hamwa na idadi kubwa ya Waislamu. Sema 'Al-hamdulillaah' unapochemua. Na umsikiapo mtu akisema hivyo baada ya kuchemua, mjibu kwa kusema: 'Yarhamukumu Allaah' (Allaah Akurehemu). Yule aliyechemua nae, na akuombee Mungu kwa kusema: 'Yahdi Kumullaah wa Yuslihu Baalakum' (Allaah Akuongoze na akusahilishie mambo yako). Kuna mahali kwingi ambako unatakiwa kusema, 'As Salaatu was Salaamu 'Ala Rasoolullaah.' Utasema matamshi hayo, kwa mfano, umsikiapo kipenzi chetu Mtume (صلى الله عليه وسلم) akitajwa jina lake au kila uingiapo au utokapo msikitini na pia uandamize matamshi haya, 'Allaahumma Iftah li abwaaba Rahmatik' na 'Allaahumma Inni As'aluka min fadhlika.'

ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO